PRESS RELEASE

PR22/265

# Bodi Tendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Yaidhinisha Mpango wa Mkopo Utakaotolewa kwa Muda wa miezi 40 wa Dola za kimarekani Milioni 1,046.4 kwa Tanzania.

- Bodi Tendaji ya IMF imeidhinisha mpango wa mkopo kwa Tanzania wenye thamani ya SDR milioni 795.58 (sawa na dola za kimarekani milioni 1,046.4, ambapo dola milioni 151.7 zitatolewa mara moja).

- Mpango huu wa ufadhili wa miezi 40 utasaidia kufufua uchumi na kukabiliana na athari za vita ya Urusi na Ukraine, kusaidia kuhifadhi uthabiti wa uchumi jumla, na kusaidia mageuzi ya kimfumo ili kuendelea kuwa na ukuaji endelevu wa uchumi wenye kuhusisha watu wote, kutokana na vipaumbele vya serikali.

- Mageuzi yatazingatia kuimarisha mfumo wa matumizi ya serikali ili kupata fedha zinazohitajika sana kwa ajili ya matumizi ya huduma za kijami na uwekezaji wa sekta ya umma wenye tija zaidi, kuanzisha tena na kuendeleza mageuzi ya kimfumo na kuimarisha na kuendeleza huduma za fedha.

**Washington, DC, Julai 18, 2021 –** Bodi Tendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) leo imeidhinisha mkopo wa muda wa miezi 40 chini ya mpango wake wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) kwa Tanzania, kwa kiwango cha SDR milioni 795.58 (sawa na asilimia 200 ya sehemu ya Tanzania IMF (Quota), sawa na dola 1,046.4 za Kimarekani). Kwa idhini hii ya Bodi, dola milioni 151.7 zitatolewa mara moja. Makubaliano chini ya mpango wa ECF yanafuatia mkopo wa dharura wa dola milioni 561.5 za Kimarekani (sawa na asilimia 100 ya sehemu ya Tanzania IMF) zilizotolewa kwa Tanzania mwaka 2021 . Makubaliano haya yanatarajiwa kuchochea upatikanaji zaidi wa misaada ya kifedha kutoka kwa nchi nyingine na mashirika mengine ya kimataifa.

Athari za vita ya Ukraine zinachelewesha kufufuka kwa uchumi wa Tanzania kutokana na janga la UVIKO-19, zimezidisha changamoto kwenye maendeleo na mageuzi ya nchi katika kufikia uwezo wake wa kiuchumi. Makubaliano chini ya mpango wa ECF yamejikita katika kusaidia kufufua uchumi kutokana na athari mbaya za janga la UVIKO-19 na kukabiliana na athari za vita ya Ukraine, kulinda uthabiti wa uchumi jumla na kuendeleza mageuzi ya kimfumo kuelekea kwenye ukuaji endelevu wa uchumi wenye kuhusisha watu wote.

Mpango huu unatokana na vipaumbele muhimu vilivyoko kwenye Mpango wa Maendeleo wa serikali wa Miaka Mitano. Msaada wa kifedha kutoka IMF unatarajia pia kusaidia kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi na kuchochea misaada zaidi ya kifedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Kufuatia mkutano wa Bodi Tendaji, Naibu Mkurugenzi Mtendaji na Kaimu Mwenyekiti Bw. Bo Li, ametoa taarifa ifuatayo.

**Muhtasari wa Maelezo ya Kaimu Mwenyekiti**

**Jamhuri ya Mungano wa Tanzania – Inaomba Mkopo wa miezi 40 chini ya Mpango wa Ukopeshaji wa ECF**

**Mkutano wa Bodi Tendaji 22/67**

**Julai 18, 2022**

Wakurugenzi watendaji wameipongeza serikali kwa namna ilivyokabiliana na hali ya uchumi kutokana na janga la UVIKO-19 na sera ilizotekeleza ili kupunguza athari kutokananavita nchini Ukraine. Wakurugenzi hata hivyo wametaja kwamba changamoto kwenye maendeleo na mageuzi pamoja na vipingamizi kutoka nje ikiwemo ni madhara ya UVIKO-19 na vita nchini Ukraine vinahatarisha kuharibu mafanikio makubwa ya uchumi yaliyopatikana kwa kazi kubwa. Kwa mtizamo huu na kutambua ufanisi mzuri wa Tanzania katika kutekeleza mageuzi, Wakurugenzi waliunga mkono maombi ya serikali kupewa mkopo wa ECF ili kukidhi mahitaji muhimu.. Walisisitiza kwamba mpango wa IMF utasaidia kuchochea misaada mingine ya kifedha kutoka nje, kusaidia kufufua uchumi huku ukiongeza fedha za matumizi kwenye huduma za kijami na maendeleo, na kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Wakurugenzi walisisitiza pia umuhimu wa kuongeza juhudi za wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19.

Wakurugenzi wamefurahishwa na dhamira ya serikali ya kusawazisha matumizi kwa kupeleka fedha zaidi kwenye huduma za kijamii na pia kuboresha ufanisi na usimamizi wake. Walihimiza kwamba ili kupata fedha zaidi kwa ajili ya matumizi muhimu ya huduma za kijamii kutahitajika kuongeza mapato ya serikali, kusimamia vizuri matumizi, na kudhibiti hasara za kifedha kwa serikali zinazoweza kusababishwa na mashirika ya umma, miradi ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi, na serikali za mitaa. Kuhakikisha hatua za kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta na vyakula zinazingatia umakini na zinakuwa za kipindi kifupi, na pia kutozidisha mikopo yenye masharti ya kibiashara litakuwa jambo muhimu ili kuhakikisha deni la taifa linaendelea kuwa himilivu. Wakurugenzi walipongeza hatua ya serikali kwenye dhamira ya kuwa na uwazi kuhusiana na UVIKO-19 na kuhimiza kuendeleza juhudi katika uwazi kwenye masuala ya mapato na matumizi ya serikali na uwajibikaji. Wakurugezi walisisitiza pia juu ya umuhimu wa kuwa na mkakati wa kujenga uwezo unaohusisha watu wote ili kurahisisha juhudi za kufikia megeuzi makubwa.

Wakurugenzi wamepongeza dhamira ya serikali kupunguza ujazi wa fedha pale itakapohitajika kufanya hivyo, huku ikiruhusu thamani ya shilingi ya Tanzania iendane na nguvu ya soko ili kupunguza athari zinazoweza kutokea. Wakurugenzi wanatarajia kuimarishwa zaidi mfumo wa sera ya fedha wa Benki Kuu ya Tanzania na kusisitiza kwamba kutahitajika mkakati mzuri wa mawasiliano. Kuboresha kanuni za fedha, usimamizi na utekelezaji wa mapendekezo ya tathmini ya sekta ya fedha ya mwaka 2018 (Financial Sector Assessment Program 2018) ni muhimu katika kukabiliana na mapungufu kwenye sekta ya fedha. Hatua zaidi zinahitajika katika kuunganisha mfumo wa kuthibiti fedha haramu (AML/CFT) na muongozo wa kikosi kazi cha kimataifa kijulikanacho kama *"The Financial Action Task Force (FATF).*

Wakisisitiza haja ya kuimarisha uwekezaji wa sekta binafsi na ukuaji wa uchumi, wakurugenzi wamehimiza serikali kutekeleza mpango wa mageuzi, ikiwa ni pamoja na kuboresha uwezo wa nguvukazi, kuongeza matumizi kwenye miundombinu, na kuondoa mwanya uliopo katika kufikia usawa wa kijinsia. Ni muhimu pia kuboresha takwimu za Pato la Taifa. Walisisitiza pia haja ya kuendelea na juhudi za kukabiliana na athari za mabadiriko ya tabia ya nchi, kwa kuanza na matokeo ya tathmini ijayo ya usimamizi wa uwekezaji wa umma unaozingatia

mabadiriko ya tabia ya nchi yaani Climate-Public Investment Management Assessment (C-PIMA).